UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

REFUGEE LAW PROJECT

# KUFANYA KAZI NA WANAUME NA WAVULANA WAATHIRIKA WA UNYANYASAJI WA KIMAPENZI NA KIJINSIA KATIKA HALI YA UKIMBIZI

## MWONGOZO WA MAMBO UNAYOHITAJI KUFAHAMISHA.

## 4

# Yaliomo

**Lengo** ........................................................................................................ 2

**Maelezo ya jumla** ........................................................................................ 3

**Ujumbe maalum kwa wafanyakazi, washirika, waathirika na jamii** ........... 4

**Mambo ya muhimu ya kuzingatia katika mpangilio wa progamu za Unyanyasaji wa Kimapenzi na kijinsia (SGBV)**.............................................. 5

**Vifaa muhimu (vya kusoma)** .................................................................. 12

# Lengo

Wanaume na wavulana wakimbizi[1] wanawezakufanyiwa unyanyasaji wa kijinsia na kimapenzi (SGBV). Waathirika wana mahitaji maalum ya kiafya, kisaikolojia, kisheria na ya kiusalama, lakini mara nyingi inakuwa vigumu kuzungumzia waliyoyapitia na kupata msaada ambao wanahitaji. Ni muhimu kwa UNHCR na washirika wake kuchukua hatua za kushughulikia matatizo haya. Malengo ya muongozo huu ni kusisitiza ya kwamba programu za kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na kimapenzi zinapashwa shirikisha wanaume na wavulana na kutoa muongozo kuhusu jinsi ya kufikia waathirika, kuwezesha utoaji taarifa, kutoa usalama na kuwafikishia matibabu ya msingi, huduma za kisheria na za kijamii. .[2]

[1]Maelezo haya yanalenga wakimbizi na inaongeleya wakimbizi mpaka mwisho. Lakini muongozo wake una maana kwa waombaji wa ukibizi , wanaorudi makwao, wenye hawana taifa, wakimbizi wa ndani kwa ndani na watu wengine ambao wanahusu UNHCR

[2] Maelezo haya yanalenga jinsi ya kufanya kazi na waathirika badala ya binu za kuzuia

# Maelezo ya jumla

Unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya wanawake na wasichana katika mazingira ya vita. Inaendelea kueleweka kama silaha ya vita[3]. Kufwatana na utetezi wa mda mrefu wa kitaifa na wa kimataifa, nchi nyingi zaidi zinatunga sheria dhidi yake, ingawaje kuzuia na kutatua bado havitoshi kabisa. Unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya wanawake na wasichana pia imekuwa jambo la muhimu kuhusu usalama katika mazingira ya ukimbizi. Kwa upande mwingine, unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya manaume na wavulana umeeleweka na kutambulika[4] kidogo.

Hata ivyo inaendelea kuwa wazi ya kwamba ni swala la usalama ambalo ni la kawaida katika mazingira ya vita na ukimbizi[5]. Inawezakuwa chanzo cha kukimbia chanzo muhimu cha mazingira magumu katika nchi ya ukimbizi. kwa wanume na wavulana wakimbizi.

Mahali ambapo kanuni za kijamii na za kitamaduni zinashinikiza utofauti wa jinsia kwa kutambulisha wanaume kama wenye nguvu na wenye kutarajiwa kulinda wanawake na watoto, mashambulizi dhidi ya alama za utambulisho wa jinsia ni silaha zenye nguvu za vita. Mahali ambapo kanuni za kijamii, na vitendo haramu kuhusu maswala ya kijinsia na muongozo wa kijinsia hutenga au hushutumu mahusiano ya jinsia moja,[6] mashambulizi ya aina ya kimapenzi dhidi ya wanaume hayatumiki kwa kupunguza uume wao mbele yao na mbele ya wakosefu, lakini yanaweza kutafsiriwa na waathiriwa, wakosefu na jamii kwa ujumla kuwa maelezo ya mwelekeo wake wa ngono (kimapenzi) au utambulishi wa kijisia[7].

---

[3] Maazimio makuu ya Baraza la usalama la Umoja wa Mataifa yanayo shughulikia Wanawake, Amani na Usalama ni 1325, 1820 na 1960.

[4] Angalia Sandesh Sivakumaran, “Lost in translation: Majibu ya Umoja wa Mataifa kwa unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya wanaume na wavlana katika mazingira ya vita, “International Review of the Red Cross, Volume 92, Number 877, March 2010”.

[5] Kwa hatua hii haiwezekani kutoa kwa ujumla, kiasi kamili sababu unyanyasaji wa kimapenzi inalipotiwa kwa kiwango cha chini na unyanyasaji dhidi ya wanaume na wavulana kwa ujumla wa unalipotiwa kwa kiwango cha chini sana. Pia kuna utafiti kidogo sana kuhusu unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya wanaume wakati wa vita (Lakini kuhusu Mashariki ya Congo angalia http/jama.amaassn.org/304/5/553.short.) Kama ilivyoonekana katika IASC Guidelines (2005): “Ni muhimu kukumbuka ya kwamba unyanyasaji wa kimapenzi unalipotiwa kidogo hata sehemu zenye vifaa vizuri vya soma kwa dunia nzima, na itakuwa vigumu kama sio kusema haiwezekana kupata vipimo vya kweli vya ukubwa wa shida kwa namna ya dharura. Kwa hiyo inawabidi wafanyakazi wa kibinadamu wote wafikirie na waamini kwamba unyanyasaji wa kijinsia (GBV) na hasa unyanyasaji wa kimapenzi unafanyika na ni tishio kubwa la usalama wa maisha, bila kizingatia kuwepo au kutokuwepo kwa ushahide wenyekuonekana.

[6] Hii mbaya sana wakati sheria ambayo inazuia uhusiano wa kimapenzi wa watu wa jinsia moja na kwa njia iliyo ya pekee wakati haiweki tofauti kati ya vitendo kwamaelewano au bila maelewano.

[7] Hii inawezakuwa uoga fulani kwa wanaume ambao wakati wa unyanyasaji wa kimapenzi walipita kuamuka kimwili kitu ambacho kwa hali hii ni jibu la mwili lakini siyo dalili ya raha ya ngono.

Unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya manaume na wavulana unahusisha vitendo vya ngono bila idhini, mukiwemo ubakaji[8], na aina mbalimbali za mateso ya kimapenzi[9]. Wanaofanya ubakaji wanawezatumia miili yao wenyewe pamoja na silaha au vitu. Zaidi ya madhara ya mwili ya hapo hapo, kitendo cha unyanyasaji wa kimapenzi inaonyesha wazi wazi uathirikaji na changamoto, jinsi anaona uume, ujinsia, uwezo wa kuzaa na utambulisho wa kijinsia[10]. Kwa hiyo waathirika wa kiume wa unyanyasaji wa kimapenzi na wa kijinsia wanaathiriwa kimwili, kisaikolojia na kijamii. Kwa waathirika wanawake, vidonda vya mwili huenda pamoja na dhiki ya kisaikolojia, majonzi, matatizo ya uhusiano wa kimapenzi, haibu za kijamii, kuwekwa pembeni na kutengwa, kutoweza kujihusisha na kazi za kiuchumi, na ukosefu wa sheria.

Kanuni za jinsia zenye mizizi imara pamoja na tabia haramu za kitamaduni na za kidini, na huduma haba hufanya vigumu kwa wanaume kueleza ya kwamba ni waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia wahudumu wanaweza kutotambua unyanyasaji wa kijinsia na kimapenzi (SGBV)[11] wa wanaume. Mara mingi jamii hazitaki kutambua yale waathirika wa kiume walipitia kwa sababu inaweza kuonekana kama kukubali udhaifu na kuaibisha jamii.

Ikibaki bila kushughulikiwa, madhara ya unyanyasaji wa kimapenzi ambayo huongeza hatari inayopatikana katika vita na mazingira ya ukimbizi inathuru ustawi wa wathirika. Mathara ya unyanyasaji wa kimapenzi kwa watu binafsi, kaya na jamii nzima yanaharibu uhusiano wa kijamii, na hivyo kudhofisha amani na usalama na uwezekano wa kufikia suluhisho za kudumu.

Unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya wanaume pia ni tishio katika mazingira ya ukimbizi. Pale ambapo wanakabiliana na changamoto kubwa za kuishi, wanaume kama vile wanawake wako kwenye hatari ya kutumiwa kwa faida ya kimapenzi na kudhulumiwa kwa malipo ya makao na chakula, au aina nyingine ya ngono kwa ajili ya kuishi. Wanaume ambao wanakabiliana na kufungwa wanawezakuwa katika hatari ya ubakaji au kuombwa fadhila za kimapenzi kwa malipo ya kuachiliwa. Hata kama mazingira ya ukikimbizi na vita ni tofauti, mahitaji ya kiusalama ya waathirika ni sawa.

---

[8] Zaidi ya wao kubakwa, wanaume na wavulana wanaweza kulazimishwa kushuhudia kubakwa kwa wao, dada zao, wasichana, mama wao na mara wanalazimishwa kubaka watu ambao wanuhusiano wakaribu nao ikiwa ni wanaume ao wanawake.

[9] Ni muhimu kujuwa kwamba waathirika wengi wanakataa kutoa maelezo kuhusu mateso ya ubakaji waliopitia

[10] Kwa taarifa zaidi kuhusu utamburisho wa jinsia, na muelekeo wa kinjinsia na mathara husika, angalia: *Working with Lesbian, Gay, Bisexual, Transgender & Intersex Persons in Forced Displacement, Need to Know Guidance 2.*

[11] Kwa nci kadhaa huduma ya matibabu kwa waathirika wa unyanyasaji wa kimapenzi inapatikana ndani ya idara cha jinakolojia.

# Ujumbe maalum kwa wafanyakazi, washirika, waathirika na jamii

- Unyanyasaji wa kimapenzi na wa kijinsia (SGBV) ni hatari kwa wanaume na wavulana vile vile kwa wanawake na wasichana. Ukweli huu lazima uonekane kwa utaratibu katika upangaji na utoaji wa mipango ya kuzuia na kujibu ikiwa ni pamoja na mipango ya kuboresha upatikanaji wa huduma za haki kwa mwathiriwa.
- Katika hali nyingi za ukimbizi, wanaume na wavulana wako kwa hatari ya kushurutishwa katika vitendo vya ngono visivyohitajika au wanaweza kulazimishwa na mazingira kufanya ngono ili waweze kuishi. Katika hali ya vita/migogoro wanaume na wavulana, kama vile wanawake na wasichana wanaweza kubakwa au kufanyiwa vitendo vingine vya aina ya unyanyasaji wa kimapenzi kama silaha ya vita.
- Wanaume wanafanyiwa unyanyasaji wa kimapenzi kama njia ya kuwanyanganya mamlaka, kuwatawala na kudhoofisha wazo la uume.
- Ubakaji ni ubakaji, haijalishi jinsia ya mwathiriwa, utambulisho wa jinsia wa kweli au ule ambao unadhaniwa au hata mwongozo wakimapenzi. Ingawa siyo kila nchi ndiyo inachukulia ubakaji wa wanaume kama kosa la jinai[12], kila mara ni ukiukwaji wa haki za binaadamu.
- Hakuna mwathirika wa unyanyasi wa kimapenzi, iwe mwanaume, mwanamke, msichana au mvulana ambaye anapashwa kufedheheshwa au kuachwa bila utunzaji
- Ingawaje katika uhusiano wa kimapenzi kwa kukubaliana kuna upatano hasa kati ya vitendo vya mtu vya ngono, kujitambua kwa mwongozo wa kimapenzi au utambulisho wa jinsia, katika mazingira ya kushurutishwa ishara hizi zinaweza kutounganishwa. Ngono ya kuingiana kwa kushurutishwa haigeuzi mwanaume au mvulana shoga, au kugeuza mwanaume kuwa mwanamke au mvulana kuwa msichana.
- Fedheha ni mmoja wapo wa vizuizi kabambe katika matibabu ya waathirika wa unyanyasaji wa kimapenzi na wa kijinsia (SGBV) kwa kuwa inaweza kuzuia waathirika kupiga ripoti na kutafuta usaidizi.

[12] Mara nyingi, maelezo ya ubakaji kwa sheria ya inchi hayahusishi wanaume.

- Kuelewa mazingira maaluma ya kanuni za jinsia ni muhimu ili kupanga usaidizi unaofaa kwa waathirika wa unyanyasaji wa kipamenzi na wa kinjinsia.
- Chanzo muhimu kinachochochea ngono kwa ajili ya kuishi kwa wanaume na wavulana pia kwa wanawake na wasichana ni ukosefu wa njia nyingine ya kuishi/maisha.
- Kutoweza kushughulikia unyanyasaji wa wanaume na wavulana inaweza kusababisha baadhi ya wathirika kutumia mbinu mbaya za kujikimu kimaisha, na katika hali mbaya mno, hua ni unyanyasaji ambao unawezakuwa na mathara ya kudumu kwenye familia na jamii kwa ujumla.

# Mambo ya muhimu ya kuzingatia katika mpangilio kamili wa progamu dhidi ya Unyanyasaji wa Kimapenzi na kijinsia (SGBV)

Wanaume na wavulana waathirika wa unyanyasaji wa kimapenzi wanateseka katika kimya kwa sababu ya kanuni za kijamii ambazo zinazingatiwa na wengi, na utambuzi wa jinsia, shutuma/fedheha za kijamii na miiko ya kitamaduni kuhusu mazungumuzo kuhusu ngono ya ujinsia hufanya vigumu kwao kwa kujitambulisha. Hata hivyo, Aidha, wakati wanazungumza, wahudumu wanashindwa kuwasikiliza au kuwaamini. Mara nyingi hawatambui ukubwa wa yale waliyoyapitia au mathara kwa ustawi wao wa baadae na uwezo wa kujitegemea. Kushindwa huku kunasababishwa na kutojali au kukosa mafunzo kuhusu kiasi gani wanaume na wavulana wanateseka kutokana na unyanyasaji wa kimapenzi na wa kijinsia, na mathara yake au jinsi mahitaji ya waathirika yanaweza kuangaliwa

Wafanyakazi na washirika ambao wanahusika na kufanya programu dhidi unyanyasaji wa kimapenzi na kijinsia wanapashwa kutambua waziwazi yale ambao waathiria wanaume na wavulana walio yapitia, heshimu haki yao ya usiri, na kuwaweka katika progamu ambazo zinazoshughulikia mahitaji yao tofauti. Kuzingatia yafuatayo itasaidia kukuza mipango ambayo inahusisha wanaume, wanawake, wavulana na wasichana.

## Kuwa makini: dalili za utambulisho

Waathirika wanaume huripoti visa vya unyanyasaji wa kimapenzi na wa kijinsia mara chache papo hapo, na mara nyiingi wanafanya hivyo tu wakati mathara ya kimwili inahitaji msaada wa haraka. Baathi ya wanauma na wavulana huthubutu kutafuta msaada miaka kadhaa baada ya tukio.

Tabia zifuatazo hazipo kila mara, lakini hata hivyo mara kwa mara wanaume waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia:

- Hawawezi kukaa na starehe; mara nyingi wanakaa kwenye ukingo wa kiti au wanaomba kusimama wakati wa mahojiano au wakati wa mkutano.Wanamaumivu ya pande ya chini ya mgongo, ambayo inaonyesha dalili za matatizo ya rektamu.
- Wanaangalia mtu usoni mara chache sana.
- Wanaonyesha kiwango kikubwa sana cha kukasirika na kuuthika.
- Wanaonyesha kiwango kikubwa sana cha ubaguzi (unaoambatana na jinsia)
- Wanaonyesha upendeleo wa nguvu wa jinsia kuhusu nani atakae mhoji.[13]
- Wanazungumza wakirudiarudia shida ambazo hazihusiane na usalama, hata kama shida kama hizo zimetatuliwa kikamilifu.

### Hatua (ya kuchukuliwa)

- Kuwa makini kwa dalili hizi na kukabiliana nazo.
- Kutoa habari kuhusu huduma za haraka, endapo inafaa, na huduma zingine ambazo zinapatika, kwa siri na kwa umakini.
- Kutoa ujumbe ya kwamba maswala nyeti yanaweza angaliwa kwa siri wakati mwathirika anajisikia kuwa tayari kwa kuongea kuhusu maswala hayo.

Kuwa makini kwa uwezekano wa kuwa unyanyasaji wa kijinsia umefanyika dhiidi ya mwanume ikiwa mwanamke ambaye amepewa ushauri anaripoti ya kwamba mpenzi wake:

- Amepoteza hamu wa kupenda mambo ya ngono na anakataa kujamiana.
- Hawezi kuhusiana na watu wengine, hata na watoto wake.
- Amejiondoa katika shughuli za kijamii na mahali pa mikutano. Tabia hii inaweza kutozungumuziwa na mwathirika, au watu wa familia wengine au marafiki.

[13] Chaguo hili linaonekana kuwa maalum kwa muathirika: wamoja wanapendelea kuhojiwa na wanume na wengine wanpendelea kuhojiwa na wanawake.

## Elewa mahitaji ya waathirika wanaume na wavulana.

Mahitaji yafuatayo ya waathirika wanaume na wavulana yanapashwa kutambuliwa na kushughulikiwa:

**Matibabu:** Madhara ya kimwili ya unyanyasaji wa kijinsia mara nyingi ni pamoja na uharibifu wa rektamu na viungo vya siri, maambukizi ya ngono na ya njia ya mkojo, na kutofanya kwa viungo vya siri. Huduma za afya zinayofaa mara nyingi hazipatikani. Maswali ya kuingilia yanayoulizwa na wafanyakazi wanaotoa huduma za afya (au hofu yake) huzuia waathirika kutafuta huduma.

**Afya ya kiakili:** Dalili za kisaikolojia ni pamoja **na** kupoteza heshima, huzuni, kukosa matumaini, wasiwasi, hasira (ikiwemo tamaa ya kujilipiza kisasi), aibu, fedheha, chuki, kumbusho[la ghafula], majinamizi, hatia, kutosikia kihisia, kukataa kuguswa, kujiondoa kwenye shughuli za nyumbani na za kijamii, uoga wa watu fulani (kama askari jeshi, polisi) ambao wanakumbusha mwathirika kuhusu watu waliowatendea makosa, matatizo ya kulala na kula**, ongezeko la matumizi ya madawa ya kulevya na pombe, na kujaribia kujiua.**

**Afya ya kijamii:** Mbali na matatizo katika mahusiano ndani ya nyumba , ikiwemo kutoroka/kuachwa na mume/mke, waathirika mara nyingi hujisikia upweke na wanaweza kufedheshwa kijamii au kutenganishwa na jamii ikiwa historia yao inajulikana. Wanweza kufukuzwa katika mahali pa kuabudu, burudani, na kazini zaidi ya kupoteza heshima nyumbani mwaao. Hofu ya kwamba hawataaminiwa inazuia waathirika wamoja kutafuta usaidizi. Waathirika wengi wanaogopa ya kwamba wao siwanaume tena, na waathirika ambao hawajaoa/olewa wanaweza kutoamini uwezo wao wa kuanzisha familia.

**Usaidizi wa mapato:** Kabla, wakati na baada ya matibabu, waathirika wengi wanajikuta hawawezi kufanya kazi inayohitaji nguvu za kimwili. Wanapopata nafuu, hasa kutoka upasuaji, waathirika wanaweza kuhitaji msaada wa mapato na wa makazi kwa muda kati ya miezi sita na kumi na miwili. Mara mwathirika anapopona ya kutosha, msaada wa kurudisha njia ya mapato inapunguza uwezekano wake wa kujihusisha katika mikakati hatari ya kimaisha.

**Usalama wa** kisheria: Ufafanuzi wa kisheria wa ubakaji mara nyingi hua ni maalum kwa wanawake na watoto, hii inafanya kuwa haiwezekani kwa watu wazima wa kiume kuandikisha mashata ya ubakaji. Kwenye uhusiano wa jinsia moja ni kosa la jinai , waathirika wanaume wanakuwa kwa hatari ya kuhojiwa kuhusu mwelekeo wao wa kijinsia na kushtakiwa kwa kujihusisha katika kitendo cha ngono ya watu wa jinsia moja. Waathirika wengi hawaripoti matukio kwa sababu hawana imani katika mfumo wa mahakama. Kushindwa kuendesha mashtaka inaweza kuongeza hatari ya kwamba makosa ya unyanyasaji wa kimapenzi na kijinsia yanaweza kurudiwa.

## Toa mafunzo ya kujumuisha kwa wafanyakazi wote kuhusu kuelewa unyanyasaji wa kimapenzi na wa kijinsia.

Kanuni za kijinsia na miiko ya kitamaduni ya wafanyakazi na wahudumu mara nyingi inafanana na ile ya waathirika. Kutoa mafunzo kamilifu kuhusu tofauti na uhusiano kati ya jinsia, ujinsia na mwelekeo wa kimapenzi na unyanyasaji wa kijinsia ni muhimu kwa wafanyakazi na washirika ikiwa wanapashwa kusikia na kushughulikia kwa makini vitendo vya unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya wanaume na wavulana, au ya hali ya unyonyaji inayoathiri wavulana na wanaume ambao wanafanya ngono ili waishi. Ni muhimu kuelewa tofauti kati ya mtu ambaye anayeshurutishwa kufanya fulani vitendo vya ngono na mwelekeo wake wa kimapenzi na utambulisho wa jinsia. Kuelewa vibaya tofauti hizo inaweza kuhatarisha nafasi ya mwanaume katika jamii yake na kuendeleza mateso yake na ya familia yake.

### Hatua ( ya kuchukuliwa)

- Chunguza na utoe changamoto kwa dhana zako wewe mwenyewe na ubaguzi kuhusu jinsia, ikiwemo wanume (katika) uathirikaji dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia na kimapenzi na madhara inayosababishwa.
- Kuendeleza uhamasishaji kupitia mafunzo, majadiliyano ambayo yanaongozwa , na utumiaji wa vifaa vinavyo imarisha uhamasishaji kama vile filamu.
- Kuanzisha mikakati ya ushirikiano na mashirika ambayo yanaujuzi maalum unaofaa.
- Kutoa mafuzo kwa UNHCR na wafanyakazi washirika, haswa kuhusu usalama, huduma muhimu na ushauri.

## Kufanya kazi na watu binafsi na kujenga imani wakati wa mahojiano.

Waathirika wengi wanachagua kutozungumzia vitendo vya unyanyasaji wa kimapenzi waliyopitia kwenye mahojiano ya kwanza. Kuchelewa kwa kuzungumza ingepashwa kuchukuliwa kama jambo kubwa na haipashwi kudhaniwa kama mtu anataka msaada zaidi au mali, au uhamiaji kwa nchi za ngambo. Waathirika wanaume wengi wanaripoti vitendo waliyopitiya waathirika wanapohitaji msaada wa matibabu wa haraka. Wakati wafanyaazi wanatambua na kushughulika katika wakati unaofaa kwa mahitaji ya kiafya hayo, imani ambayo wanajenga maranyingi huwezesha wanaume na wavulana kuzungumzia wazi vitendo vya unyanyasaji wa kimapenzi waliyopitia.

**Hatua (ya kuchukuliwa)**

- Kuwa makini kwa dalili (ona ukurasa wa 6)
- Inapo wezekana mwathirika achague ikiwa atahojiwa na mwanaume au mwanamke. [14] Wakati mwathirika ni mdogo, mhoji anapashwa kupewa mafunzo haswa kuhusu kuhoji watoto
- Kwenye utafsiri unahitajika, ruhusu mwathirika kuchagua mtafsiri anayependelea.
- Elezea mwathirika ya kwamba vile anafafanua yale aliyoyapitia vizuri ndivyo kesi yake itaeleweka, na ya kwamba mikutano ya kufuatilia inawezekana..
- Uliza kama mtu huyo anamahitaji ya matibabu ya haraka ambayo yanahitaji kuangaliwa.
- Heshimu masimulizi ya mwathirika na upambanuzi wake, na uhakikishe na uonyeshe wazi ya kwamba imefanya hivyo kwa kuandika na kumrudiria yale amezungumza. Usijaribu kufasilia yale aliyoyapitia (kwa mfano, ubakaji kama unyanyasaji) Kwenye inawezekana na kwa makubalino, endeleza ushauri wa kibinafsi na uongeze watu ambao wanawezakusaidia kama vile bibi/bwana, watu wengine wa familia,familia zinazomuhifadhi ili kutoa usaidizi kamili kwa watu binafsi ambao wameathirika.
- Tambua uhalali wa hisia za hasira, na uchunguze jinsi gani mwathirika anaweza kuelekeza hisia hizi vizuri.
- Elezea waathirika ya kwamba vitendo vya ngono kwa kushurutishwa haihusiane na mwelekeo wake wa kimapenzi

## Kutoa msaada wa waathirika wenzi.

Waathirika wengi wanajaribu kukabiliana peke yao, bilakujua ya kwamba waathirika wengine wanawezakuwa na shida kama zao au zenyeuhusiano kama wao. Kuunda kikundi cha waathirika kama wao inawezakuwa ni kuimarisha na kuponya kwa sababu watu wanaweza kutambua shida zao kwa ujumla. Vikundi vinahitaji mbinu za kujihadhari, na haswa kuhusu siri.

[14] Ingawaje waathirika wengi watapendelea mhoji wa jinsia moja nao, hii haifanyiki kila mara. Wakati wowote ikiwa inawezakana wanapashwa kupewa fursa ya kufanya chaguo

**Hatua (ya kuchukua)**

- Toa nafasi ya usalama abamo vikundi vinaweza jiunda na kukutana. Wapeni shauri na usaidizi.
- Ambia waathirika ya kwamba waliotumwa na wahudumu ya kwamba kuna kikundi cha kujitegemea.
- Imarisha vitendo vya kujisaidia (kwa mfano kuwezesha wanamemba kusaidiana kupitia kujuliana hali  hospitalini).
- Ruhusu wanamemba kutuma waathirika kupata msaada wa ushauri na wa kisheria.

## Eleza wakimbizi na jamii zao ya kwamba UNHCR inaelewa unyanyasaji wa kijinsia na wa kimapenzi (SGBV) kwa kikamilifu

Jamii yote inapashwa kufahamu na kuwa makini kuhusu mambo yanayohusu unyanyasaji wa kijinsia na kimapenzi (SGBV). Inapashwa elewa ya kwamba katika watu ambao wanawezakuwa waathirika kunapatikana wanaume. Wananume na wavulana wanapashwa kujua ya kwamba tishio au tendo la unyanyasaji wa kimapenzi dhidi yao inatambuliwa na inaeleweka. Wanawake na wasichana wanapashwa kujua ya kwamba ndugu na marafiki wao wa kiume wanaweza kuathirika na unyanyasaji wa kijinsia na wa kimapenzi na ya kwamba matokeo yake yanachukuliwa na umuhimu na ya kwamba yatashughulikiwa kwa siri.

**Hatua (ya kuchukuliwa)**

- Weka mabango na vipeperushi kwenye maeneo muhimu kama vile vyumba vya kukaa kungojea, vyumba vya mikutano, na vyumba vya ushauri. Vijikaratasi hivi vinapashwa:
    - Kuonyesha ya kwamba wanume na wavulana kama wanawake na wasichana ni waathirika.
    - Orodhesha huduma na habari ya mawasiliano kwa wale wanaohitaji msaada.
- Endesha mikutano inayolenga kupasha habari na vikundi vya wakimbizi na jamii zao ukieleza aina tofauti za unyanyasaji wa kimapenzi, hali hatarishi ya pamoja na ile maalum ya wanawake, wanaume, wavulana na wasichana, na orodha ya huduma za usaidizi ambazo zinapatikana kwa waathirika na familia zao.
- Saidia vikundi vya wakimbizi kuitoe mafunzo zaidi kwa jamii zao.

## Anzisha kanuni za utaratibu wa uendeshaji wa kazi (SOPs)

Weka mifumo wazi na kamilifu ya kutuma ili kutoa huduma ambayo waathirika wanawake na wanaume wanahitaji. Aina na kasi ya kutuma itaboreka ikiwa zinatumia protokali wazi, kwa njia ya kanuni taratibu za uendeshaji wa kazi (SOPs).[15]

### Hatua (ya kuchukua)

- Anzisha protokali wazi au SOPs, zilizokubaliwa na pande zote.
- Hakikisha ya kwamba inaeleza na kufafanua wajibu wa kila sekta na majukumu ya wahusika muhimu.
- Hakikisha ya kwamba inahitaji kushirikiana na kujumuisha jamii.
- Hakikisha ya kwaba utekelezaji wake unafuatiliwa mara kwa mara.
- Hakikisha kuna usiri.

## Imarisha usalama kwa waathirika wanaume na wavulana

Wakati mathara ya unyanyasaji wa kimapenzi yanayoonekana mara nyingi ni ya kimwili na ya kisaikolojia, matatizo yanayohusika na usalama yanahitaji kushughulikiwa.

### Hatua (ya kuchukua)

- Tumia mbinu za Age, “Gender and Diversity” ( Umri, Jinsia na Anuai) [16] wakati wa kufanya mipango yote ya usalama na ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia na wa kimapenzi.
- Hakikisha ya kwamba kazi na waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia na wa kimapenzi wa kiume imezingatiwa katika kanuni za utaratibu wa uendeshaji wa kazi (SOPs) za unyanyasaji wa kimapenzi na kijinsia (SGBV) zote nchini na mbinu husika.
- Hakikisha ya kwamba bajeti za progamu dhidi SGBV zina fedha maalum za kusaidia kwa garama za matibabu na za huduma za kisaikolojia ya waathirika na mahitaji yao ya msingi wakati wanapata nafuu (chakula, makazi).

[15] Baathi ya wahusika, kwa mfano mashirika ya huduma za afya, yanaweza kuwa na sekta za maalum za SOPs au protokali kushughulikia aina maalum za dhuluma. Kwa kesi kama hizo hii inapashwa kuwekwa kama kiambatisho kwa SOPs.

[16] Kama ilivyoandikwa katika “Age, Gender and Diversity Policy” ya UNHCR ya mwaka wa 2011: Kufanya kazi na watu na jamii kwa usawa na usalama.

- Weka unyanyasaji wa kimapenzi dhidi ya wanaume na wavulana katika mafunzo kuhusu SGBV kwa ma afisa wa mahakama, polisi, magereza na ma afisa wa vituo vya vizuizini, viongozi wa ma kambi, wafanyakazi, washirika na wengine.
- Tafuta wahudumu ambao wana moyo wa huruma na uwezo na weka njia maalum ya kutuma (kesi) kwao ambayo, ikiwa lazima inapashwa kutofautisha kijinsia.
- Hakikisha ya kwamba vikundi ambavyo vinafanya kazi inayoambatana na usalama na unyanyasaji wa kimapenzi na wa kijinsia (SGBV) vina ufahamu kuhusu unyanyasaji wa kimapenzi na kijinsia dhidi ya wanaume na ya kwamba inafikia ajenda inayotoa mwelekeo tawala kwa tatizo.
- Tumia vikundi vinavyohusika na kazi ya usalama kuanzisha njia ya kutuma (kesi) kwa waathirika wote wa unyanyasaji wa kimapenzi na kijinsia, iliyotofautishwa na jinsia na umri inapobidi. Jiusishe na wanasheria (wabunge) na njia zingine za sera kuimarisha ufafanuzi wa ubakaji unyanyasaji wa kimapenzi ikiwemo kufanya ubakaji wa wanaume kosa la jinai.
- Anzisha uhusiano ili kutambua na kuchunguza kesi za kufungwa kwa wakimbizi na waomba hifadhi bila mashtaka katika vituo vya kuzuiliwa na magerezani.

# Vifaa muhimu (vya kusoma)


- IASC, Guidelines for Gender-Based Violence Interventions in Humanitarian Settings: Focusing on Prevention of and Response to Sexual Violence in Emergencies, Geneva (2005). At: www.humanitarianinfo.org/IASC/downloaddoc.aspx?docID=4402

- Rome Statute of the International Criminal Court(1998).At http://www.icc-cpi.int/NR/rdonlyres/ADD16852-AEE9-4757-ABE7-9CDC7CF02886/283503/RomeStatutEng1.pdf

- UNHCR, Operational Protection in Camps and Settlements. A Reference Guide of Good Practices in the Protection of Resources and Other Persons of Concern (June 2006). At http://www.unhcr.org/refworld/docid/44b381994.html.

- UNHCR Age, Gender & Diversity Policy, working with People and Communities for Equality and Protection (2011). At: http://www.unhcr.org/refworld/docid/4def34f6887.html

- UNHCR, Heightened Risk Identification Tool (HRIT) (2010). At: http://www.unhcr.org/refworld/docid/4c46c6860.html
- UNHCR, Action against Sexual and Gender-Based Violence: An Updated Strategy (June 2011). At: http://www.unhcr.org/refworld/docid/4e01ffeb2.html

- UNHCR, Sexual and Gender-based Violence Against Refugees, Returnees and Internally Displaced Persons: Guidelines for Prevention and Response (May 2003). At: http://www.unhcr.org/refworld/pdfid/3edcd0661.pdf

- WHO, Ethical and Safety Recommendations for Researching, Documenting and Monitoring Sexual Violence in Emergencies, Geneva (2007). At: http://www.who.int/gender/documents/OMS_Ethics&Safety10Aug07.pdf


Websites

- http://www.refugeelawproject.org
- http://www.stoprapenow.org
- http://www.rhrc.org
- http://clinicalcare.rhrc.org/docs/facguide.pdf